**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU -**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2026**

**RUANGWA-LINDI**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu:0785 921 99**
**Mkuu wa Shule: 0785 921 995**
**Makamu Mkuu wa Shule-Utawala: 0713 608897**
**M/Mkuu wa shule-Taaluma:0620449686**
**Matron/Patron: 0674 604 729**

**Shule ya Secondary: MANDAWA**
**S.L.P: 02 RUANGWA.**
**Tarehe ......................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi .....................................**
**S.L.P.......................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MANDAWA HALMASHAURI YA RUANGWA MKOA LINDI MWAKA.............................**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka................ na atasoma tahasusi ya.........................

Shule ya Sekondari **MANDAWA** ipo umbali wa Kilometa **39** kaskazini mwa Mji wa **Ruangwa.** Usafiri wa basi kutoka mjini: **Ruangwa** unapatikana katika kituo cha mabasi cha **Ruangwa stendi**. Panda basi na ufike moja kwa moja Ruangwa mjini stendi ya mabasi. Kisha panda gari linaloelekea moja kwa moja mandawa kwa nauli ya Tsh. 7,000/=. Kisha utachukua pikipiki (bodaboda) na kukupeleka moja kwa moja Mandawa sekondari kwa nauli ya tsh. 3,000/=

Muhula wa Masomo unaanza tarehe................, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ................ Mwisho wa kuripoti ni tarehe **........................**

**1. Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

**1.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni **suruali mbili(02) nyeusi** za kitambaa cha suti **Esteem no.1** kwa **wavulana** na

Sketi **mbili (02) nyeusi** kitambaa cha suti **Esteem no.1** kwa **wasichana**.

Maelezo ya mshono: **Urefu unao gusa kiatu na upana wa heshima iwe na malinda mawili kwa mbele na mfuko mmoja nyuma, pindo la inchi 18-19 miguuni bila turn up** kwa wavulana na **sketi ndefu inayoishia Katikati ya magoti na makanyagio kwa wasichana**.

ii. Mashati **meupe mawili (02) ya mikono mirefu na yenye kola shingoni na ziwe na vishikizo vya kawaida si vya chuma.**

iii. Sare ya Michezo ni **bukata moja na t-shirt moja isiyo na kola ya blue** na **tracksuit ya dark green moja(01)** na **viatu vya michezo (njumu kwa ajili ya mpira pair 01 na raba nyeusi pair 01 kwa ajili ya jogging**. Na soksi nyeusi ndefu kwa ajili ya michezo kwa wote.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana za shule;

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Sweta **rangi ya kijivu lenye kola ya ”V” moja(01)**

viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) **suruali mbili (02) rangi ya ugoro** kitambaa cha suti **Esteem no.1 ndefu kugusa kiatu na upana wa heshima** kwa wavulana na **sketi mbili (02) rangi ya ugoro** kitambaa cha suti **Esteem no.1** ndefu kufika Katikati ya magoti na makanyagio kwa wasichana na fulana **rangi ya kijivu zenye nembo ya shule mbili (02)** zenye kola kwa wote. (***Zina patikana shuleni)***

Gauni rangi ya damu ya mzee (maroon) na juba lake kwa waislamu wakike.

ix. Tai **mbili(02) ndefu rangi NYEUSI**

x. Tisheti (T-shirt) :**Rangi ya dark green za darasani yenye nembo ya shule mbili (02)** kwa wote. (*Zina patikana shuleni)*

***Nb: kwa wale wanaovaa juba, hakikisha juba lako linakuwa la stara (heshima) na rangi iwe sawa na sare unayovaa juu. Mfano juba jeupe kwa shati nyeupe, na juba dark green kwa t-shirt ya dark green.***

***ANGALIZO: HAKIKISHA UNAVAA SARE ZA SHULE WAKATI WOTE UWAPO NJE NA NDANI YA SHULE, NGUO ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI SHULENI NA USIJE NAZO.***

## 1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo:-

i. Madaftari **Countebook quire 4 (yasipungue 11)** ;

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);

iv. Scientific Calculator; na Dissecting kit kwa wanafunzi wa PCB, PCM na CBG.

v. Godoro la sponji moja 2½, x 6

vi. Shuka mbili (2) za rangi ya **bluu Bahari** na foronya zake kwa **wavulana**, pia Shuka mbili (2) za rangi ya **pink** na foronya zake kwa **wasichana**, blanket 1 dark blue, foronya ya godoro 1 kwa wote, na chandarua 1 (blue kwa wavulana, pink kwa wasichana).

vii. Nguo za ndani za kutosha;

viii. Taulo

ix. Vitenge viwili (02) kwa wasichana

x. Sabuni za kuogea na kufulia za kutosha

xi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

xii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

**xiii. VIFAA VYA USAFI**

a) Tahasusi ya CBG,PCB na HGK walete kwanja 1, squizer 1, fagio wa ndani (soft broom) na sabuni ya maji lita 5 na ARO kwa ajili ya kusafishia sink za choo

b) Tahasusi ya PCM,PGM na HGL walete jembe 1. reki 1, fagio wa chelewa 1, sabuni ya maji lita 5 na ARO kwa ajili ya kusafishia sink za choo

**NB: KAMA HANA BIMA YA AFYA, AJE NA TSH. 50,400/= KWA AJILI YA BIMA (Hii isiingizwe kwenye akaunti aje nayo mkononi)**

### 1.3 Michango mbalimbali

Mzazi/mlezi utachangia michango ifuatayo kupitia akaunti Na. **71101100102** jina la akaunti : **MANDAWA SECONDARY SCHOOL RECURRENT ACCOUNT -NMB**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| **Jumla** | | **80,000/=** |

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali/dawa bila idhini
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

MKUU WA SHULE
MANDAWA SEKONDARI
S.L.P 02
ANGWA - LINDI

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule : BOAZ TITUS MAGANGA**
**Mhuri wa Mkuu wa Shule :**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0785921995**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0713608897**
- **Mwandamizi Taaluma : 0625772212**
- **Mwandamizi Malezi : 0695 341 984**

# RUANGWA DISTRICT COUNCIL
# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**THE HEADMAS**
**MANDAWA SECONDARY SC**
**P O**

MKUU WA SHULE
MANDAWA SEKONDARI
S.L.P 02
RUANGWA - LINDI

**DATE………………**

**TO:**

**The Medical officer**

**……………………………………**

**Re: NAME……………………………………..**

Please examine the above as to his/her physical and mental fitness for full time course of Secondary education at Mandawa Secondary School.

1. Eye sight……………………………………………………………………………..
2. Hearing……………………………………………………….……………………..
3. Speech…………………………………………………………………………………
4. Venereal diseases ……………………………………………………………………
5. Neurosis……………………………………………………………………………..
6. TB……………………………………………………………………………………….

Doctor's Remarks…………………………………………………………………….

Doctor's Advice………………………………………………………………………

Doctor's Name..........................................................................................................

Signature……………………………Rubber stamp………………………………………

Date……………………………………………

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

**SHULE YA SEKONDARI MANDAWA**

**FOMU YA KUJIANDIKISHWA SHULENI NA TAARIFA ZA MZAZI NA MWANAFUNZI.**

**SEHEMU A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili ……………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa …………………………………………………
3. Kabila …………………………..

4. Mahali na Wilaya alipozaliwa …………………………………………………..

5. Shule alipomaliza Darasa la Saba ……………………………………………….

6. Kidato anachokuja kuingia ………………………………………………….

7. Michezo anayopendelea

| | |
|---|---|
| 1 | |
| 2 | |
| 3 | |

**UONGOZI WA SHULE**

Kazi yoyote ya uongozi aliyowahi kufanya kama vile. Kiranja, Kiongozi wa Kwaya, Ngoma Michezo n.k.

| S/N | NAFASI YA UONGOZI | SHULE | MWAKA |
|---|---|---|---|
| **1** | | | |
| **2** | | | |
| **3** | | | |

Nathibitisha kwamba habari zilizotolewa hapo juu ni kamili na za ukweli

**Tarehe ……………..      saini…………………………..**

**SEHEMU B: TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

i. Jina kamili...........................................................................

ii. Kazi..................................................................................

iii. Nyumbani..........................................................................

iv. Kata...................................................................................................

v. Tarafa................................................................................................

vi. Anwani ya Mzazi/Mlezi ………………………………………………..

vii. Namba ya simu ……………………….

viii. Dini…………………………

ix. Anuani kamili ya nyumbani ambako mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo…………………………………………

Ninaahidi kushirikiana na Walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapakazi na mwenye bidii ya kusoma.

Mimi …………….Mzazi/Mlezi wa……………… ninathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi

Tarehe ………………………  saini……………………………..

**MKATABA WA MWANAFUNZI KUHUSU KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi ……………………………nimeyasoma kwa makini maelezo haya ya kujiunga na shule. Kwa hiari yangu nakubaliana nayo.

Naahidi nitaheshimu sheria, kanuni na taratibu zote za shule na miongozo mbalimbali itakayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Aidha naahidi kuwa kwa vyovyote vile sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai nikiwa shuleni au nje ya shule.

Endapo nitavunja sheria, kanuni, taratibu za shule, kushiriki katika migomo, fujo na kutenda makosa ya jinai, basi nichukuliwe hatua stahiki kulingana na kosa nitakalokuwa nimefanya.

Saini ya Mwanafunzi.......................................................................

Saini ya Mzazi..............................................................................



Saini ya Mkuu wa shule :

MKUU WA SHULE
MANDAWA SEKONDARI
S.L.P 02
RUANGWA - LINDI

Mhuri wa mkuu wa shule:

**ORODHA YA VITABU VINAVYOHITAJIKA**

## GEOGRAPHY PAPER 1

1. Principles of of physical geography by – F.J Monkhouse
2. A comprehensive approach to physical geography for secondary – by D.T Msabila
3. Practical geography for Africa – By John M. Prichard
4. Landforms in Africa – an introduction to geomorphology by colin buckle

## GEOGRAPH PAPER 2

1. Human and economic geography – by Goh cheng & Morgan
2. Advanced level geography course book – by Tanzania institute of education (TIE)

3. An integrated focal regional studies on human and economic geography advanced level paper II by D.T Msabila.

## VITABU VYA BIOLOJIA: -

1. .Gleen and Toole (1999). *Understanding Biology 4th Edition*.Stanlye Thomes LTD UK.
2. Kent M. (2013). *Advanced Biology*.Oxford University Press LTD 2nd Edition
3. Aggarwal S. (2017). *A text book of CBSE.Biology for Class XI*.Nijra Publishers and Printers PVT.LTD
4. Verma P. S and Pandey BP (2012). *S. Chands Biology for class VI.*Chand and Company LTD.New Delh
5 Verma P. S and Pandey BP (2012). *S. Chands Biology for class VII*.Chand and Company LTD.New Delh
6 Taylor etal (1997) *Biological Science.3rd Edition,* Cambridge university Press LTD.
7 T.I.E (2019) *Biology for Advanced Level Secondary School.Student's Book Form Six,* Dar es salaam, T.I.E
8 T.I.E (2019) *Biology for Advanced Level Secondary School.Student's Book Form Five,* Dar es salaam, T.I.E

**VITABU VYA PHYSICS:**

1. Mehta, R. and V. K Mehta (2009) *"Principles of Physics for Class XI*" New Delhi, S.Chand and Company Ltd.
2. Nelcon, M and P. Parker (1995) *"Advanced level Physics''* 07th Edition, London, Heinmann Educational books.
3. TIE (2019) "*Physics for Advanced Level Secondary Schools*, Form Five, Dar es salaam, TIE.

## VITABU VYA ADVANCED MATHEMATICS

1. Mathematics, For Class XI, Volume I, S. CHAND
2. Mathematics, For Class XI, Volume II, S. CHAND
3. Mathematics, For Class XII, Volume I, S. CHAND
4. Mathematics, For Class XII, Volume ii, S. CHAND
5. Pure Mathematics 1, 3rd edition, Backhouse, J.K, Houldsworth, S.P.T, B.E.D(1985)
6. Pure Mathematics 2, 3rd edition, Backhouse, J.K, Houldsworth, S.P.T, B.E.D(1985)

# VITABU VYA CHEMISTRY

1. Jain s.k (2006) *Conceptual Chemistry XI ,4th edition*. Chand, New delhi India
2. Ngaiza lusima (2014) *Atomic Structure and Bonding*. Hopegen company ltd. Dar es salaam. Tanzania
3. Ngaiza lusima (2014*) Physical Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania
4. Ngaiza lusima (2014) *Inorganic Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania
5. Ngaiza lusima (2014) *Environmental and Soil Chemistry*. Hopegen Company Ltd. Dar es salaam. Tanzania.
6. E. Ramsden (2001) *Calculations for A-level chemistry*.

**Muhimu:**

**Nunua vitabu vinavyotolewa na Taasisi ya elimu Tanzania, kwa kila somo unalosoma**

**MUONGOZO WA SARE NA MAVAZI YANAYONUNULIWA NJE YA SHULE**

| | | |
|---|---|---|
|  |  |  |

| Shati jeupe la darasani | Rangi ya suruali na sketi ya darasani (black) | Rangi ya tie |
|---|---|---|
|  **Rangi ya suruali na sketi ya kushindia** |  **Rangi ya shuka na foronya lake kwa wavulana** |  **Rangi ya tracksuit** |
|  **Raba nyeusi** |  **Rangi ya gauni na juba lake** |  **Rangi ya shuka na foronya lake kwa wasichana** |